



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
MKOA WA GEITA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE  
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Kumb. Na. E.40/13/35

17/01/2022

## YAH: TANGAZO LA KAZI.

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mpya chenye Kumb. Na. FA.170/521/01 "B"/81 ya tarehe 6 Desemba, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe anawatangazia wataanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi za kazi zifuatazo;-

### 1. Katibu Mahsusi III TGS B<sub>1</sub> (Nafasi 01)

#### *Sifa ya Mwombaji*

- i. Awe amefaulu Elimu ya Kidato cha Nne
- ii. Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu
- iii. Awe amefaulu somo la Hatimkato la Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- iv. Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program Windows, Microsoft Office, Internet, E – Mail na Publisher.

### 2. Kazi na majukumu ya Katibu Mahsusi III TGS B<sub>1</sub>;

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- Kusaidia kutunza kumbukumbu, taarifa za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa Wasaidizi wake na pia kumuarifu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa waliopo katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**3. Masharti ya waombaji wote;-**


- Kila mwombaji ahakikishe anaambatanisha vivuli vya vyeti vyake halisi vya kidato cha nne, vyuo na cheti cha kuzaliwa.
- Kila mwombaji aambatanishe nakala ya taarifa binafsi (CV).
- Kila mwombaji aambatanishe picha za rangi (Passport Size 2 zenye jina la mwombaji nyuma).
- Awe raia wa Tanzania
- Awe hajawahi kupatikana na makosa ya jinai na kuhukumiwa
- Asiwe na umri wa miaka zaidi ya 45
- Asiwe amewahi kuachishwa kazi kwa makosa ya nidhamu na kughushi vyeti.
- Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya matokeo ya kidato cha nne **HAVITAKUBALIWA**
- Waombaji watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili
- Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatahuhulikiwa

Ikumbukwe kuwa kuwasilisha vyeti vya uongo vya elimu na ujuzi (Forgery Certificates) ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za Nchi.

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 20/02/2022 saa 9:30 jioni.** Maombi yote yanaweza kuandikwa kwa Kiswahili au kiingereza na kuwasilishwa Ofisi ya Masjala Bayana iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe au kutumwa posta kwa anwani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya,  
S. L. P 02,  
**BUKOMBE**

**Imetolewa na;**



Lutengano G Mwalwiba  
Mkurugenzi Mtendaji (W)

**BUKOMBE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**BUKOMBE.**